بِسْمِ اللهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيْمِ

**Yaliyomo** **Ukurasa**


**i.** Utangulizi..........................................................................................2

**ii.** Uhakika wa kujibiwa Dua………………………………….…..……...2

**iii.** Dua ya Kufungua Baraka…….………………………………………4

**iv.** Dua ya Kuomba kupata Mapenzi ya Allah na kuwa Mja mwema…………………………………………………….……………..4

**v.** Dua ya Kufungua Rizki……………………………...……………..6

**vi.** Dua ya Kuomba Kupata Mali ya Halali …………..……...…....7

**vii.** Dua ya kufanikisha mambo yako yote ……………..…..……11

**viii.** Dua unapokwenda Msikitini………………………………..…...12

**ix.** Kumtoa Jini ndani ya mwili wa Mwanaadamu……………13

**x.** Dua ya Kuondosha Balaa…………………………………………16

**xi.** Kuwapatanisha wanao gombana……………….……....…...…16

**xii.** Njia ya kufanya Istikhara…………………..……………………...18

**xiii.** Dua ya kumrejesha Mke au Mume……………………….……20

**xiv.** Dua Ukiwa na Haja/Shida kwa Mtu……………………...……27

# UTANGULIZI

Alhamdulillaahi; Sifa njema zote Anastahiki Allah (Subhaanahu wa Ta'aala) Mola wa Viumbe wote, Rehema na Amani zimshukie kipenzi chetu Mtume Muhammad (Swalla Allahu Alayhi wa Sallam) na Swahaba zake (Radhwiya Allahu Anhum) na waliowafuata kwa wema mpaka siku ya mwisho.

Kitabu hiki ni muendelezo wa kitabu chetu kilichopita ambapo ni mkusanyiko wa Dua tukufu zenye majibu ya haraka.

Ikumbukwe kuwa Dua maana yake ni mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Mja na Mola wetu Mlezi, Muumba wetu, Mwenye kujua, na Mwenye nguvu. Ibada ya Dua kwa ujumla wake ni kuimarisha, kuwezesha, kukomboa au kubadilisha na ni kitendo chenye nguvu kiibada ambacho Muumini anaweza kufanya. Dua imeitwa silaha ya Muumini nayo inathibitisha imani ya mtu kwa Mungu Mmoja na inazuia aina zote za ibada za Sanamu au Ushirikina. Dua kimsingi ni utii kwa Mwenyezi Mungu na udhihirisho wa haja ya mtu kwa Mwenyezi Mungu.

## UHAKIKA WA KUJIBIWA DUA

Maulamaa wote wanakubaliana kuwa kheri yote huwa ni sababu ya kuridhika Mwenyezi Mungu na mja wake na shari yote inatokana na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu juu ya mja wake.

Ikiwa kheri yote inatokana na kuridhika kwa Mwenyezi Mungu na mja wake, kwa hivyo funguo za kheri ni Dua pamoja na unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu na kuonesha kumpenda kwa kutenda yale yanayomridhisha na kumuogopa kwa kuepukana na makatazo yake.

Mja anapokabidhiwa Ufunguo huu (Ufunguo wa kuomba Dua) na Mola wake basi ajue kuwa Mola wake anamtakia kheri na anaponyimwa Ufunguo huu basi ajue kuwa amefungiwa mlango wa kheri.

Anatufundisha Amir-ul-Muminiin Ally Bin Abi Twalib (Radhwiya Allahu Anhu) Kwamba;

"Anayejaaliwa vitu vinne hanyimwi vinne:-

i. Anayejaaliwa kuomba Dua hanyimwi kukubalika kwake;
ii. Anayejaaliwa kufanya Toba hanyimwi kukubalika kwake;
iii. Anayejaaliwa kuomba Msamaha hanyimwi kusamehewa kwake;
iv. Anayejaaliwa kutoa Shukurani zake hanyimwi kuongezewa kwake."

Basi na tumuombe Allah (Subhaanahu wa Ta'aala) atujalie kuwa miongoni mwa waja walio kabidhiwa Ufunguo huu wa kuomba Dua na kupata majibu, Aamiin.

# DUA YA KUFUNGUA BARAKA

**UTARATIBU;**

- **Soma kila siku Jina hili tukufu la Allah (Subhaanahu wa Ta'aala), Mara mia moja ishirini na tisa (129) tu;**

يَا لَطِيْفُ

**YAA LATWIIF**

- **Kisha soma Aya hii tukufu kwa idadi hiyohiyo ya mara mia moja ishirini na tisa (129) tu;**

اللّٰهُ لَطِيْفٌ بِعِبَادِهِ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْقَوِيُّ الْعَزِيْزُ

**ALLAHU LATWIIFUN BI 'IBAADIHI, YARZUQU MAN YASHAA-'U, WA HUWA L'-QAWIYYU L-'AZIIZ**

- **Kisha soma Majina haya Matukufu ya Allah (Subhaanahu wa Ta'aala) Mara ishirini na moja (21) tu;**

يَا كَافِى يَا غَنِيُّ يَا فَتَّاحُ يَا رَزَّاقُ يَا كَرِيْمُ
يَا وَهَّابُ يَا ذَا الطَّوْلِ يَا مُجِيْبُ

**YAA KAAFII, YAA GHANIYYU, YAA FATTAAHU, YAA RAZZAAQU, YAA KARIIMU, YAA WAHHAABU, YAA DHAL TTWAULI, YAA MUJIIBU**

- **Dumu na uradi huu na baada ya muda mfupi baraka zitakushukia na kipato chako kitaongezeka kwa idhini ya Allah (Subhaanahu wa Ta'aala).**

# DUA YA KUOMBA KUPATA MAPENZI YA ALLAH (SUBHAANAHU WA TA'AALA)

**UTARATIBU;**

- **Soma Dua hii mara moja (1) kila baada ya swala ya faradhi. Dua hii ni ya kuomba kheri, huruma na mapenzi kutoka kwa Allah (Subhaanahu wa Ta'aala) huku ikiondosha shari zote za Walimwengu.**

بِسْمِ اللهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيْمِ

اللَّهُمَّ إِنِّى أَسْأَلُكَ حُبَّكَ وَحُبَّ مَنْ يُحِبُّكَ وَحُبَّ عَمَلٍ يُقَرِّبُنِى إِلَى حُبِّكَ ، اللَّهُمَّ مَا رَزَقْتَنِى مِمَّا أُحِبُّ فَاجْعَلْهُ قُوَّةً لِى فِيْمَا تُحِبُّ ، وَمَا زَوَيْتَ عَنِّى مِمَّا أُحِبُّ فَاجْعَلْهُ فرَاغًا لِى فِيْمَا تُحِبُّ ، اللَّهُمَّ اجْعَلْ حُبَّكَ أَحَبَّ إِلَيَّ مِنْ أَهْلِيْ وَمَالِى وَمِنَ الْمَاءِ الْبَارِدِ عَلَى الظَّمَأِ ، اللَّهُمَّ حَبِّبْنِى إِلَيْكَ وَإِلَى مَلَائِكَتِكَ وَأَنْبِيَائِكَ وَرُسُلِكَ وَعِبَادِكَ الصَّالِحِيْنَ ، وَاجْعَلْنِى مِمَّنْ يُحِبُّكَ وَيُحِبُّ مَلَائِكَتَكَ وَأَنْبِيَاءَكَ وَرُسُلَكَ وَعِبَادَكَ الصَّالِحِيْنَ ، اللَّهُمَّ أَحْيِ قَلْبِى بِحُبِّكَ وَاجْعَلْنِى لَكَ كَمَا تُحِبُّ ، اللَّهُمَّ اجْعَلْنِى أُحِبُّكَ بِقَلْبِى كُلِّهِ ، وَأُرْضِيْكَ بِجُهْدِى كُلِّهِ ، اللَّهُمَّ اجْعَلْ حُبِّى كُلَّهُ لَكَ ، وَسَعْيِى كُلَّهُ فِى مَرْضَاتِكَ.

**ALLAHUMMA INII AS-ALUKA HUBBAKA WAHUBBA MAN YUHIBBUKA WAHUBBA 'AMALIN YUQARRIBUNII ILAA HUBBIKA, ALLAHUMMA MAA RAZAQTANII MIMMAA UHIBBU FAJ-'ALHU QUWWATAN LII FIIMA TUHIBBU, WAMAA ZAWAYTA 'ANNII MIMMAA UHIBBU FAJ-'ALHU FARAAGHAN LII FIIMAA TUHIBBU, ALLAHUMMA J-'AL HUBBAKA AHABBA ILAYYA MIN AHLII WAMAALII WAMINALMAAILBAARIDI 'ALAA ADHWAMAI, ALLAHUMMA HABBIBNII ILAYKA WA ILAA MALAAIKATIKA WA ANBIYAAIKA WARUSULIKA WA 'IBAADIKA SSWAALIHIINA, WAJ-'ALNII MIMMAN YUHIBBUKA WAYUHIBBU MALAAIKATAKA WA ANBIYAAIKA WARUSULAKA WA 'IBAADAKA SWAALIHIINA, ALLAHUMMA AHYI QALBII BIHUBBIKA WAJ-'ALNII LAKA KAMAA TUHIBBU, ALLAHUMA J-'ALNII UHIBBUKA BIQALBII KULLIHI, WAURDHWIIKA BIJUHDII KULLIHI, ALLAHUMA J-'AL HUBBII KULLAHU LAKA, WASA'A YII KULLAHU FII MARDHWAATIKA.**